HISTORIA YA DHAMANA YA UWEKEZAJI TANZANIA
(UNIT TRUST OF TANZANIA)

Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) iliundwa mnamo tarehe 19 Juni, 2003. Imeundwa chini ya Sheria ya Udhamini, Sura ya 375 ya Sheria za Tanzania. Ili kuweza kutambua malengo na shughuli za Dhamana ya Uwekezaji Tnzania ni muhimu kwanza kabisa kuelewa msingi wa Dhana ya udhamini kwa lugha ya kigeni - "TRUST". Katika kila udhamini, kuna pande tatu zinazotambulika kisheria na kiutekelezaji.

- "MUANZISHAJI WA DHAMANA" (kwa lugha ya kigeni akiitwa "SETTLOR") -Huyu ni mtu binafsi au taasisi inayeweka mali chini ya uangalizi ya wadhamini katika dhamana.

- "WADHAMINI" (kwa lugha ya kigeni "TRUSTEES") – Hawa ni waangalizi wa mali iliyowekwa na "muanzishaji wa dhamana".

- "WANUFAIKA" (kwa lugha ya kigeni "BENEFICIARIES") - Ni watu wambao mali inawekwa mikononi mwa Wadhammini (Trustees) kwa ajili ya manufaa yao.

Mbali na wahusika katika mpangilio wa udhamini, pia kuna MALI ambayo ndiyo kiini cha Dhamana ambayo huitwa kisheria kama mali katika udhamini (kwa lugha ya kigeni "PROPERTY" au "CORPUS OF THE TRUST").

Muanzishaji wa Dhamana" (Settlor) wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwakilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha.
Wadhamini wa sasa ni:

Balozi E. A. Mulokozi	-	Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini
Mhe. J. J. Akukweti (Mb)	-	Mdhamini
Balozi F. D. Mbaga	-	"
Bibi K. S. Mbatia	-	"
Bibi E. J. Manyesha	-	"

Wanufaika wa Dhamana ya Uwekezaji ni raia wa Tanzania. Mali au kiini katika Dhamana ya Uwekezaji ni hisa ambazo zimetunzwa chini ya dhamana hiyo pamoja na haki zinazoambatana na hisa hizo.

Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ilianzishwa kama mrithi wa taasisi ambayo hapo awali ilijulikana kwa jina la Dhamana ya Ubinafsishaji (Privatization Trust (PT)). Dhamana hiyo ya Ubinafsishaji ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge iliyotungwa kwenye mwaka 1997. Malengo ya Dhamana ya Ubinafsishaji yalikuwa:-

(a) Kupata hisa katika mashirika yaliyobinafsishwa kwa ajili ya kuuzwa kwa umma ili kupata mgawanyo mpana miongoni mwa raia na kupata faida kulingana na hali ya wakati huo;

(b) Kuhamasisha na kuunda mazingira ya kuongeza ushiriki mpana zaidi wa raia katika umiliki wa mashirika yaliyokuwa yamebinafsishwa;

(c) Kuwa na uwajibikaji katika ulipaji wa faida kulingana na Sheria ya Ubinafsishaji;

(d) Kumshauri Waziri na Tume juu ya masuala yanayohusiana na utekelezaji wa Sheria;

(e) Kudhibiti na kuendesha Dhamana kwa lengo la kuhakikisha kwamba malengo ya dhamana yanafikiwa;

(f) Kuhakikisha kwamba hisa zinauzwa na kugawanywa kutegemeana na hali halisi, kwa mwekezaji halali.

Baada ya kuanzishwa, Dhamana ya Ubinafsishaji Tanzania ilipewa sehemu ya hisa za Kampuni ya Bia Tanzania (Tanzania Breweries Ltd.) na Kampuni ya Sigara Tanzania Cigarette Co. Ltd. Hisa hizi ziliwekwa zikisubiri kuuzwa kwa umma. Zaidi ya hapo, Dhamana ya Ubinafsishaji ilikwishafanya maandalizi ya uanzishwaji wa Mipango ya Uwekezaji wa Pamoja. Pia iliendesha mipango ya elimu kwa umma kwa kushirikiana na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) pamoja na Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Sekta ya Umma (PSRC).

Baada ya muda wa Dhamana ya Ubinafsishaji kumalizika, shughuli zake zilichukuliwa rasmi na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania. Sheria ya Dhamana ya Ubinafsishaji muda wake ulikwisha tarehe 14.06.2003 na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania iliandikishwa tarehe 19 Juni, 2003. Ni muhimu kusema kwamba kuanzishwa kwa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania, kulikwisha bashiriwa na Sheria ya Dhamana ya Ubinafsishaji ya mwaka 1997 ambayo iliweka utaratibu wa kurithiwa kwake na Mpango wa Amana 1(Unit Trust). Kwa hali hiyo, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ni taasisi ambayo imeanzishwa hivi karibuni, ambayo kwa sasa inaweka misingi kwa ajili ya mustakabali wa shughuli za aina nyingi hapo baadaye.

MALENGO YA DHAMANA YA UWEKEZAJI TANZANIA

Malengo ya Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ni:-

(a) Kupokea na kutunza katika dhamana hisa za mashirika yaliyobinafsishwa zilizokuwa zimeshikwa na Dhamana ya Ubinafsishaji, na hisa zote za mashirika yaliyobinafsishwa zitakazowekwa katika Dhamana na Serikali kama muanzishaji wa Dhamana katika zoezi zima la ubinafsishaji wa mashirika ya umma.

(b) 1. Kifungu 8(1) cha Sheria ya Ubinafsishaji ya 1997 kilieleza kwamba ‘kama kufikia mwisho wa kipindi cha dhamana, Dhamana ya Ubinafsishaji bado itakuwa inashikilia hisa, basi Bodi ya dhamana itaibadilisha dhamana hiyo kuwa mpango wa amana (unit trust)”.

(b) Kuhakikisha kwamba hisa zilizo katika dhamana, zinagawanywa miongoni mwa raia wa Tanzania kwa njia ile itakayowezesha uwekaji wa akiba na ushirikishwaji mpana wa raia katika umiliki wa mashirika yanayobinafsishwa utakaowezesha ushiriki katika masoko ya mitaji.

(c) Kuanzisha na kuendesha mipango ya uwekezaji wa pamoja ili kufikia malengo ya Dhamana.

Ni dhahiri kwamba malengo haya yanahusisha uwezeshaji. Uwezeshaji ni dhana pana ambayo inaweza kutekelezwa kwenye sekta mbali mbali za kitaifa kwa mipango ya aina nyingi. Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ni Taasisi iliyopo kwenye sekta ya fedha, hivyo mipango yake shurti iendane zaidi katika mipango ya kifedha ya kuwawezesha Watanzania kuendesha shughuli mbali mbali za kiuchumi. Katika kuanzisha shughuli za Dhamana ya Uwekezaji, mtazamo wa awali umewekwa katika uanzishwaji wa mpango wa uwekezaji wa pamoja (Collective Investment Scheme) utakaojulikana kama Mfuko wa Uwekezaji wa Umoja (au kifupi kwa lugha ya kigeni “UMOJA FUND”).

Malengo ya Dhamana ya Uwekezaji yameelezwa kwa makini zaidi hapa chini.

KUPOKEA NA KUTUNZA HISA ZA AMANA (WAREHOUSING OF SHARES)

Tangu mwanzoni mwa miaka ya themanini, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikitekeleza mpango wa ubinafsishaji wa mashirika ya umma. Mashirika kadhaa ya Umma yamekwisha binafsishwa na mengine yakijumuisha yale ya huduma muhimu yanaendelea kubinafsishwa. Baadhi ya mashirika yaliyobinafsishwa yameweza kujiendesha kwa faida na mengine tayari yameorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE). Watanzania wengi wamepewa nafasi ya kumiliki baadhi ya hisa za mashirika yaliyouzwa ikiwa ni pamoja na hisa za Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC), Kampuni ya Saruji Tanga (SIMBA) na Kampuni ya Usafirishaji wa Mizigo ya Uwanja wa Ndege Dar es Salaam (DAHACO).

Ukubwa wa Makampuni yanayobinafsishwa unaweza kwa wakati fulani kuzidi uwezo wa kuyabinafsisha kwa kutumia Soko la Hisa pekee. Kwa kushughulikia tatizo hili mpango wa utunzaji wa hisa bakaa katika ghala maalum la hisa ulianzishwa. Hisa za namna hiyo hutunzwa wakati zikisubiri muda muafaka wa kuziuza kwa wananchi kwa njia mbali mbali.

Katika tarehe ya makala hii, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania inazo hisa 23,594,272 za Kampuni ya Bia Tanzania, na hisa 3,000,000 za Kampuni ya Sigara Tanzania. Hisa hizi zitatumiwa kama mbegu ya mitaji kwa mipango mbali mbali ya

uwekezaji wa pamoja itakayoanzishwa siku za baadaye. Kwa muktadha huu, Dhamana inapanga kufanya kazi na makundi mbali mbali ya jamii katika kuanzisha mipango maalum iliyokusudiwa. Dhamana ya Uwekezaji inaanzisha mpango wa Kitaifa utakaojulikana kama Mpango wa Uwekezaji wa Umoja au "Mfuko wa Umoja" na baada ya hapo itashirikana na washikadau wengine kuanzisha mipango mingine.

Dhamana ya Uwekezaji imependekeza na Serikali imekubali utaratibu maalum kwa ajili ya umiliki mpana wa hisa kwa wananchi wa Tanzania. Hii inahusisha Serikali kutoa hisa za Makampuni yaliyobinafsishwa kwa mipango ya uwekezaji wa pamoja kama Mbegu ya Mtaji. Baadaye amana za mipango hiyo zitatolewa kwa raia wa Tanzania kwa bei iliyopunguzwa na ambayo Watanzania walio wengi wataimudu.

Inategemewa kwamba, siku za baadaye, Serikali itaongeza hisa za Mashirika mengine ya umma katika Dhamana ya Uwekezaji. Uzoefu wa Dhamana ya Uwekezaji katika kutumia hisa zilizopo hivi sasa utatumika kama kigezo mhimu katika maamuzi ya Serikali kuweka hisa zingine za mashirika kwenye Dhamana ya Uwekezaji.

KUWEZESHA UMILIKI MPANA WA HISA MIONGONI MWA WATANZANIA

Serikali imeazimia kwamba Watanzania lazima wapewe nafasi ya kumiliki hisa, hasa zile za mashirika yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE). Idadi kubwa ya Watanzania imeweza kupata hisa za TBL, TCC, SIMBA na DAHACO. Mbali na kuwezesha umiliki wa hisa hizo, Watanzania wamefaidi chemichemi za gawiwo kutokana na hisa hizo pamoja na kupanda kwa bei za hisa hizo.

Hatua kubwa zimechukuliwa katika kuhamasisha umiliki mpana wa hisa kupitia Soko la Hisa. Hata hivyo, vizuizi fulani vya kimuundo vinafanya kuwa vigumu kwa Watanzania walio wengi kushiriki katika Soko la Hisa. Dhamana ya Uwekezaji inaanzisha muundo mbinu ambao utawawezesha Watanzania wengi zaidi kushiriki katika umiliki wa hisa. Kwa muktadha huu, utaratibu ni kuleta soko karibu kabisa kwa watu ili kwamba waweze kuuza na kununua amana wakiwa katika maeneo yao. Dhamana ya Uwekezaji inakusudia kufanya hivyo kwa kukamilisha makubaliano ya uwakala na mabenki pamoja na taasisi za fedha ambazo zina mtandao mpana nchini.

Moja ya malengo ya Serikali ni kuwezesha umiliki wa hisa miongoni mwa Watanzania. Kupata hisa za makampuni yaliyoorodheshwa na DSE ni njia mojawapo ya kuwezesha umiliki mpana wa hisa. Njia nyingine kadhaa zinaweza kubuniwa. Njia moja bora ni kupitia katika uanzishaji wa mipango ya uwekezaji wa pamoja. Mipango hii, hutoa nafasi kwa wawekezaji mbali mbali ikiwa ni pamoja na wawekezaji wa kipato cha chini kushiriki katika kuwekeza fedha kidogo walizo nazo na kupata faida za kuweka pamoja rasilimali katika mipango hiyo. Kwa hiyo basi, Dhamana ya Uwekezaji imepewa jukumu la kuwezesha umiliki mpana wa hisa miongoni mwa Watanzania. Moja ya njia muhimu za kufikia umiliki mpana wa hisa ni katika kuhamasisha na kuendesha mipango ya uwekezaji wa pamoja.

KUKUZA NA KUENDESHA MIPANGO YA UWEKEZAJI WA PAMOJA

Kisheria, mpango wa uwekezaji wa pamoja umeelezwa kama:-

(a) Kampuni ya Uwekezaji wa wazi (open-ended investment company);

(b) Mpango wa amana (unit trust scheme);

(c) Mipango mingine inayohusu mali ya aina yoyote ikiwa ni pamoja na fedha, kusudi au matokeo yake iwe kuwezesha watu kushiriki katika mpango (iwe ni kwa njia ya kuwa na umiliki wa mali au sehemu yoyote ya mpango au vinginevyo) kushiriki katika au kupokea faida au mapato yanayotokana na upataji, utunzaji uendeshaji au utoaji wa mali au jumla ya fedha iliyolipwa kutokana na faida au mapato;

(d)Mpango wowote au mpangilio uliokusudiwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana.

Maelezo haya, ni wazi kwamba yanaweza kuonekana kuwa ni magumu kwa watu ambao hawana ujuzi wa kisheria. Hata hivyo, cha msingi katika maelezo haya ni kwamba mipango ya uwekezaji wa pamoja inajumuisha ukusanyaji au uwekaji wa rasilimali pamoja kutoka katika wawekezaji mbali mbali na kuziwekeza rasilimali hizo kwenye amana mbali mbali. Katika tafsiri hii, mtu angeweza kusema kwamba kampuni yeyote basi ni chombo cha uwekezaji wa pamoja kwani kunakuwa na wanahisa wengi. Mpango wa uwekezaji wa pamoja unadhihirisha tofauti kadhaa kuhusiana na mtazamo huu.

Kwanza, lengo la uwekezaji kwenye mpango wa uwekezaji wa pamoja ni maalumu – kuwekeza katika amana zinazouzika. Lengo hili huwapa wawekezaji faida ya ukwasi ambayo ni muhimu (hasa kwa mipango ile inayosemekana ni ya wazi (open-ended) yaani amana zake zinaendelea kununuliwa na kuuzwa kila mara)2 . Kumbuka, mtu hawezi kununua hisa za kampuni na tena akapendekeza kuuza hisa hizo katika kampuni hiyo. Kwa upande wa mpango wa uwekezaji wa pamoja, hili linawezekana.

Pili, kuna tofauti fulani za kimuundo. Mpango wa amana (ambao ni aina moja wapo ya mpango wa uwekezaji wa pamoja) unaye Meneja ambaye siyo mwana kikundi au mbia. Meneja huyu hufanya shughuli zake kitaaluma kulingana na sheria. Itakumbukwa kwamba Meneja wa Kampuni ya kawaida huteuliwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni na anawajibika kwa Bodi.

2. Katika mpango wa namna hii, muwekezaji anaweza kununua na kuuza amana (units) kwa Meneja wa mpango kwa muda wote ambao mpango utakuwepo. Mauzo na manunuzi yanaendelea kwenye muda wa biashara wakati wowote.

Zaidi ya hapo Kampuni inaendeshwa na wamiliki wa hisa. Mbadala na hivyo, mpango wa uwekezaji wa pamoja unaendeshwa na Meneja anayeshirikiana na mlinzi malum wa mpango (custodian)3 . Meneja anafanya shughuli zake chini ya misingi ya kisheria ikihusisha nyaraka za uanzishaji wa mpango (Trust Deed) pamoja na sheria za nchi.

Tatu, kuna tofauti muhimu katika njia ya kuthamini mali ya mpango wa uwekezaji wa pamoja na ile ya kampuni. Uthamini wa mali mbali mbali za kampuni ni jambo tata na wakati mwingine, ni vigumu kuthamini mali fulani (e.g. nia njema [good will]). Kutokana na aina ya rasilimali inayowekezwa katika mipango ya uwekezaji wa pamoja yaani amana zinazouzika, uthamini unakuwa na wepesi wa aina fulani – kufuata thamani halisi ya rasilimali hizo kwenye soko. Kwa kawaida uthamini huu hufanywa kila siku ya biashara.

Kama vile orodha katika tafsiri ya Mpango wa Uwekezaji wa Pamoja unavyoeleza, mipango mbali mbali inaweza kuanzishwa. Mpango uliozoeleka katika uwekezaji wa pamoja ni MPANGO WA AMANA (Unit Trust Scheme); ambayo pia unajulikana kama Mfuko wa Pamoja (Mutual Fund), katika lugha ya Marekani na nchi nyingine kadhaa.

Mipango ya uwekezaji wa pamoja inafanya kazi kwa kanuni ya ukusanyaji wa rasilimali ikiweka rasilimali hizo mikononi mwa wenye taaluma za utawala na uwekezaji wa fedha na kuruhusu wawekezaji kushiriki katika kupata faida zinazotokana na uwekezaji wa fedha zilizokusanywa kwenye mfuko mmoja. Kwa maana halisi, mipango ya uwekezaji wa pamoja inatoa faida zifuatazo:-

- Kukusanya akiba ndogo ndogo kuwa fedha nyingi iliyokusanywa kwenye mfuko mmoja (pooling resources into a fund)4 ;
- Matumizi ya taaluma kwenye utawala wa fedha zilizokusanywa5 ;
- Wasiwasi wa hasara (risk) uliosambazwa katika amana mbali mbali zinazo nunuliwa na fedha nyingi iliyokusanywa kwenye mfuko mmoja6 ;
- Gharama ndogo za wawekezaji (lower transaction costs)7 ; na
- Uwezo wa kufikia uwekezaji wa viwango vya juu (access to investment in higher thresholds)8

3. Meneja wa mpango ni Mshauri wa uwekezaji aliyepewa liseni ya kufanya shughuli hiyo. Meneja huyu huingia Mkataba maalum (nyaraka za udhamini) na mtunzi maalum wa mpango (kwa lugha ya kigeni akiitwa “custodian”). Meneja anaendesha mpango na mtunzi anatunza mali ya mpango.

4. Badala ya kila mtu kuweka nyumbani TShs. 10,000/= kwa sababau ni kidogo sana kuwekezwa, watu 10,000 wangewekeza kiasi hicho na kujenga mfuko mkubwa wa kiasi cha TShs. 100,000,000/=. Fedha zilizopo kwenye mfuko huu huwekezwa na faida inayopatikana kugawanywa kwa wale wawekezaji wadogo kutokana na kiasi walichowekeza.

5. Kuwekeza kwenye mfuko unaoendeshwa kitaaluma huhakikisha kwamba zinawekezwa ipasavyo kwa faida ya waekezaji.

6. Meneja mwenye taaluma huweza kutengeneza mchanangnuo wa uwekezaji ambao unapunguza wasiwasi wa hasara (risk). Kama muwekezaji akiwekeza kwenye dhamana moja tu, ikipata hasara basi ni hasara ya moja kwa moja. Lakini akiwekeza kwenye dhamana bali mbali basi hasara katika moja inaweza kufutwa na faida kutoka kwa nyingine. Hii inadhihirisha msemo kwamba

7. Muwekezaji binafsi mwenye fedha chache hulipa gharama kubwa zaidi za uwekezaji kuliko Meneja mwenye mfuko mkubwa na taaluma ya uwekezaji. Meneja huyu huweza kulipa kamisheni chache na vile vile huweza kupata riba kubwa zaidi kutoka kwenye taasisi za fedha.

8. Muwekezaji mwenye TShs. 10,000/= hawezi kuwekeza kwenye uwekezaji unaohitaji kwa uchache TShs. 100,000,000/=. Meneja aliyekusanya fedha kutoka kwa wawekezaji wengi na aliye na mfuko mkubwa huweza kufanya hivyo.

9. Mfano hai wa namna ambavyo vyombo vya uwekezaji wa pamoja vinavyofanikisha uwezeshaji ni ule wa Ghana ambako chombo maalum cha kukopesha fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba (Housing Finance Company of Ghana) kiligundua kwamba wateja walikuwa wanashindwa kukopa kwa sababu ya kukosa mtaji wa mwanzo wa asili mia kumi (10%). Taasisi hiyo ilianzisha mpango wa amana ili kuweza kujenga mazingira ya kuweka akiba na wateja waweze kukidhi malipo ya asili mia hiyo.

“usiweke mayai yote kwenye kapu moja”. .

Uhamasishaji na uanzishaji wa mipango ya uwekezaji wa pamoja wa Dhamana ya Uwekezaji, utatoa faida hizo kwa Watanzania.

Hakuna mpango wa uwekezaji wa pamoja uliyowahi kuanzishwa Tanzania na hivyo ni wakati muafaka kwamba Dhamana ya Uwekezaji lazima ichukue jukumu la kutoa faida zilizotajwa hapo juu kwa Watanzania. Nchi zingine ambamo mipango hii imekuwa ikitumika ni pamoja na Afrika Kusini, Zimbabwe, Zambia, Ghana, Mauritius na hivi karibuni Kenya.

MIPANGO YA UWEKEZAJI WA PAMOJA NA UWEZESHAJI

Mengi yanazungumzwa kuhusu mipango ya uwekezaji wa pamoja na sera ya uwezeshaji wa wananchi. Kwa hali hiyo ni wajibu kwamba uhusiano wa mambo haya mawili uwekwe wazi. Uwezeshaji unahusiana na ushiriki wa makusudi wa makundi ya jamii katika uchumi wao na maendeleo endelevu ya uchumi wa kitaifa na upatikanaji wa faida inayotokana na shughuli za kiuchumi kwenye jamii. Je, Mipango ya uwekezaji wa pamoja inaletaje uwezeshaji9?

Kwanza, inawawezesha watu wa kipato cha chini kuwekeza rasilimali ndogo ndogo walizonazo. Kipengele hiki siyo tu kinatoa matumaini mahali pa kukata tamaa kwa wawekezaji wadogo, bali pia kinatoa nafasi ya kupatikana faida za kiuchumi baada ya muda. Faida kutoka katika mipango hii ya uwekezaji, inaweza kuwa kichocheo kikubwa cha uwekaji akiba kwa wale wenye vipato vidogo.

Pili, Mipango ya uwekezaji wa pamoja inawezesha wawekezaji wote wakubwa pamoja na wadogo kusambaza wasiwasi wa hasara (risk diversification) kwa kuwekeza katika amana mbali mbali. Wawekezaji wa kipato cha juu wanaweza kupata msaada wa nyongeza kutoka kwa washauri wa uwekezaji na kuweza kukidhi mahitaji ya lengo hili. Kwa hali hiyo faida inayotolewa kwa wawekezaji wa kipato cha chini na mpango wa

uwekezaji wa pamoja ni kubwa. Kusambazwa kwa wasiwasi wa hasara hutoa kinga ya nyongeza ukilinganisha na wasiwasi huo ambao haukusambazwa.

Tatu, mipango ya uwekezaji wa pamoja hutoa faida kutegemea na vivutio vilivyopo. Faida inaweza kuwa katika mgawanyo wa mapato ya mpango (income distribution) (ambayo ni sawa na ulipaji wa gawio kwenye kampuni) au inaweza kuchukua mfumo wa uongezekaji thamani ya mtaji (capital appreciation). Ikiwa mpango unaogawanya mapato unawawezesha wawekezaji kuwekeza tena kiasi ambacho kingegawanywa (re-investment) nafasi kubwa inatolewa ya wawekezaji kukuza mtaji wao. Kutokana na gharama kubwa za uendeshaji katika baadhi ya rasilimali, haiwezekani kwa wawekezaji wa kipato cha chini kuwekeza tena. Mpango wa uwekezaji wa pamoja unatoa nafasi hiyo.

Nne, mwekezaji katika mpango wa uwekezaji wa pamoja anastahili kupata amana zinazoitwa kwa lugha ya kigeni Units. Units zinaweza kuhamishika. Units pia zinaweza kutumika kama rehani (collateral) ili kumwezesha mwekezaji kupata mkopo. Sasa hili ni muhimu sana pale washiriki mmoja mmoja wa makundi ya jamii wanazo units na wanataka kusaidia miradi katika maeneo yao. Inawezekana kwa units walizonazo kukusanywa ili kufikia thamani ya kuifaidisha miradi mikubwa. Katika mazingira ya Dhamana ya UwekezajiTanzania, faida nyingine muhimu inabidi itajwe. Serikali inafuatilia dondoo ya uwezeshaji na njia moja inayokusudia kutumia ni kusaidia mipango iliyoanzishwa na Dhamana ya Uwekezaji. Msaada unaweza kuchukua sura mbili ambazo ni punguzo katika bei katika matoleo ya awali (Initial Public Offer) kwa umma pamoja na msamaha wa kodi Ni kwa ajili ya sababu zilizotajwa hapo juu kwamba uanzishwaji wa mipango ya uwekezaji wa pamoja umepewa kipaumbele katika hatua hii ya mwanzo ya kazi ya UTT.

DHAMANA YA UWEKEZAJI KAMA TAASISI YA FEDHA

Mbali na malengo ya Dhamana ya Uwekezaji yaliyotajwa hapo juu, wadhamini wamepewa pia kazi fulani ambazo kwa kawaida hufanywa na taasisi za fedha. Miongoni mwa nyingine kadhaa, hizi zinajumuisha;

(a) Kutunza, kuendesha au kufanya mipango ya uwekezaji kwa kadiri itakavyowezesha usambazaji wa hisa zilizo katika amana kwa njia ile itakayoongeza thamani, faida au mapato yake.
(b) Kuwekeza, kupata, kutunza na kutoa amana na kutumia uwezo na haki zinazotokana na amana hizo.
(c) Kutoa mikopo yenye rehani ya mali yoyote isiyohamishika inayohamishika.

(c) Kupokea, kukusanya, kununua, kuuza kupatanisha au vinginevyo kushughulikia hati yoyote ya kubasilishana (bill of exchange), hati za mikopo ya fedha, hati za ahadi ya kulipa deni, kuponi, hati za mikataba, hati za kusafirishia mali toka nje ya nchi, hati yenye mamlaka juu ya mali, waranti, vyeti na nyaraka nyinginezo za biashara.

(d) (e) Kununua kuuza au kutoa hati za ushiriki kuhusiana na mkopo wowote, au fedha zilizotolewa na taasisi ya fedha au benki au taasisi nyingine ya namna hiyo.

(f) Kuwekeza katika hati yeyote maalum au amana iliyotolewa na Serikali, Benki Kuu au Serikali za mitaa.

(g) Kubuni kuhusiana na mpango wowote wa uwekezaji wa pamoja;

(i) Uwekaji wa akiba na mipango ya bima au mipango ambapo mtu anaweza kupata riba katika kushirikiana na kampuni ya bima lakini isiyojumuisha biashara ya bima.

(ii)

(ii) Mpango mwingine wowote au mipango itakayomwezesha mtu kupata riba katika units.

(h) Kupata mali isiyohamishika au masilahi kwenye umiliki wake (maendeleo ikiwa ni pamoja na ujenzi) na kuuza mali hiyo.

(i) Kutoa huduma ya biashara ya kibenki na huduma za uwekezaji

(j) Kutoa huduma za uwekezaji wa kifedha, fedha au amana kwa mtu yeyote ndani na nje ya Tanzania.

(k) Kununua au kuuza au kuingia katika shughuli nyingine ya ubadisilishaji wa fedha za kigeni kwa kadiri itakavyolazimu kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake.

(l) Kufanya aina yoyote au biashara inayohusu ukusanyaji wa akiba au uwekezaji ambao mwekaji wa mali katika dhamana anaweza kuruhusu; na

(m) Kufanya kwa ujumla matendo yote na vitu vitakavyojitokeza au kutokana na utendaji wa kazi zake chini ya amana.

Kazi hizi zimewekwa kwa Dhamana ya Uwekezaji ili kuiwezesha kukamilisha malengo yaliyotajwa hapo mwanzoni mwa makala hii. Kwa mfano, wakati wowote, Dhamana ya Uwekezaji itakuwa na rasilimali ya muda mikononi mwake (rasilimali ambazo zinasubiri kutumika katika mipango mbali mbali ya baadaye). Dhamana ya Uwekezaji Tanzania haiwezi kuruhusu rasilimali hizo zikae tu bila kutumika. Lazima ziwekezwe. Na zinaweza kuwekezwa katika njia mbali mbali za uwekezaji. Baadhi ya mipango ya uwezeshaji inaweza kuhusisha utoaji wa misaada mbali mbali ya kifedha itakayotolewa na Dhamana yenyewe au katika ushirikiano na taasisi zingine za fedha. Nyingine zinaweza kuhusisha utumiaji wa hati za biashara. Dhamana ya Uwekezaji vile vile inaweza kumiliki mali. Dhamana ya Uwekezaji pia inaweza kufanya huduma za kifedha za aina mbali mbali.

MPANGO WA KAZI WA MUDA WA KATI WA DHAMANA YA UWEKEZAJI

Dhamana ya Uwekezaji imetengeneza Mpango wa Kazi wa Muda wa Kati (Medium Term Work Plan) wa shughuli zake. Katika kutengeneza mpango huo, Dhamana ya Uwekezaji imezingatia uzoefu wa urekebishaji wa uchumi nchini ikiwa ni pamoja na ubinafsishaji, uboreshaji wa uchumi kwa ujumla, maendeleo katika masoko na mitaji, uelimishaji wa umma juu ya nafasi za uwekezaji n.k.

Mpango wa kazi wa muda wa kati, umefafanuliwa katika mipango ya utekelezaji inayojumuisha yafuatayo:-

(a) Uanzishaji wa mipango ya uwekezaji wa pamoja;
(b) Kuzingatia sheria;
(c) Uimarishaji wa uwezo na mafunzo;
(d) Maendeleo ya miundombinu;
(e) Elimu kwa umma;
(f) Udhibiti wa hisa zilizo kwenye amana.

MUUNDO WA DHAMANA YA UWEKEZAJI

Dhamana ya Uwekezaji Tanzania inatambua kwamba majukumu na shughuli zake ni ya muda na hapo hapo kwamba taasisi ambazo itakuwa imezianzisha na kuziendeleza ni za kudumu. Kwa hiyo Dhamana ya Uwekezaji imetengeneza muundo ambao ni wa wazi kuhusiana na uwajibikaji kwa shughuli zake. Zaidi ya hayo, muundo umeandaliwa kwa jinsi kwamba taasisi zitakazoanzishwa na Dhamana ya Uwekezaji, zitakuwa na uwezo siku za usoni wa kujiendesha zenyewe. Hii ina maana kwamba zitakuwa na uwezo wa kujiendesha kama asasi za kibiashara.

DIRA NA DHAMIRA ZA DHAMANA YA UWEKEZAJI TANZANIA

DIRA

KUWA TAASISI YA UWEKEZAJI YENYE UFANISI AMBAYO ITAENDELEZA UBINAFSISHAJI NA KUWAWEZESHA WATANZANIA KUWA WASHIKADAU KATIKA MAENDELEO YA UCHUMI WA NCHI YAO KWA AJILI YA KUBORESHA HALI YAO YA MAISHA NA UCHUMI WA NCHI.

DHAMIRA

- KUTUNZA NA KUDHIBITI HISA ZA MAKAMPUNI YALIYOBINAFSISHWA KATIKA DHAMANA KWA AJILI YA WATANZANIA.

- KUWEZESHA UTAMADUNI WA KUWEKA AKIBA MIONGONI MWA WANANCHI WA TANZANIA.

- KUWEZESHA UMILIKI MPANA WA HISA ZA MASHIRIKA YALIYOBI NAFSISHWA NA MAKAMPUNI MENGINE MIONGONI KWA
  WATANZANIA

- KUANZISHA NA KUENDESHA MIPANGO YA UWEKEZAJI WA PAMOJA.

HITIMISHO:

Dhamana ya Uwekezaji sasa imejiandaa kuanza kazi. Lengo kuu la sasa ni kuanzisha Mfuko wa Umoja ("Umoja Fund"). Taratibu nyingine za kifedha zitaandaliwa na kutekelezwa kwa uangalifu na tahadhari yakizingatiwa mahitaji ya makundi ya jamii yasiyo na uwezo wakiwemo wanawake, vijana n.k.

Makala ya Habari kwa Umma namba 2 itatoa habari juu ya mpango wa kwanza wa uwekezaji wa pamoja katika Tanzania.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na:-

Afisa Mtendaji Mkuu
Dhamana ya Uwekezaji Tanzania
Jengo la Sukari, Ghorofa ya Tatu
S. L. B. 14825
Dar es Salaam
Simu Na.+255-22-2122501/2137592
Faksi Na: +255-22-2137593
Barua pepe: ubinafsishaji@yahoo.com